# Utata baina ya Dhana za Unyambulishaji na Uambatizi katika Ufafanuzi wa Sarufi ya Kiswahili

*Luinasia Elikunda Kombe*
*Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam*

**Ikisiri**

**Makala hii imelenga kuibua utata uliopo baina ya dhana za unyambulishaji na uambatizi katika mofolojia ya Kiswahili. Unyambulishaji na Uambatizi ni dhana zinazohusu michakato ya uundaji wa maneno. Mgawanyo wa dhana hizi ulifanywa kwa kutumia chujio la lugha za Ulaya ambazo mofolojia yake ni tofauti na mofolojia ya lugha za Kibantu (Kosch, 2011). Hivyo, dhana hizo zinapotumika katika ufafanuzi wa sarufi ya lugha za Kibantu, kikiwemo Kiswahili, hubua utata. Makala hii imebaini kwamba utata huo husababishwa na mambo matatu. Kwanza, ni suala la dhima za viambishi vya unyambulishaji na uambatizi kuingiliana. Pili, ni suala la nafasi ya viambishi vya unyambulishaji na uambatizi katika mzizi au shina la neno. Tatu, ni kuwepo kwa istilahi tofauti tofauti zinazotumiwa na wanaisimu wa Kiswahili kurejelea dhana hizo. Makala hii imefafanua mambo hayo kwa kina na kuonyesha namna yanavyosababisha utata baina ya dhana ya unyambulishaji na uambatizi.**

**Maneno Muhimu**: *Unyambulishaji, Uambatizi, Uambishaji, Mzizi, Viambishi*

**Utangulizi**

Makala hii imelenga kubainisha namna dhana za unyambulishaji na uambatizi zinavyoibua utata katika ufafanuzi wa sarufi ya Kiswahili. Ili kufikia azma hii, makala imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza ni utangulizi ambao unafasili baadhi ya istilahi, sehemu ya pili inahusu mjadala wa mambo yanayoleta utata kuhusu dhana ya unyambulishaji na uambatizi na sehemu ya tatu ni hitimisho.

Maumbo mengi ya maneno ya Kiswahili huundwa na mzizi au shina na viambishi (Ashton, 1947). Miongoni mwa maneno ambayo kwa kiasi kikubwa mizizi au mashina yake huweza kubeba viambishi ni vitenzi, nomino na vivumishi (Nkwera, 1989). Viambishi hivyo vinaweza kuwekwa kabla na baada ya mzizi au shina (Nkwera, 1989; Kihore na wenzake, 2003; Massamba, 2004) kwa kutaja wachache. Tazama mfano ufuatao:

**Mfano 1: Muundo wa maneno ya lugha ya Kiswahili**

| | **Shina la neno** | **Shina au Mzizi na Viambishi** |
|---|---|---|
| (a) | cheza | **a**-**na**-**wa**-chez-**esh**-a |
| (b) | pika | **si**-pik-**i** |
| (c) | refu | refu-**sh**-**a** |
| (d) | soma | som-**o** |
| (e) | mtoto | **m**-toto |

Katika mfano huu Na. 1, vijipande vya maneno vilivyokolezwa wino ni viambishi, ilhali sehemu iliyobaki ni mzizi au shina. Katika mfano (1a) na (b) viambishi vimetokea kabla na baada ya mzizi. Katika mfano (1c) na (1d) viambishi vimetokea baada ya mzizi au shina na katika (1e) kiambishi kimetokea kabla ya shina. Kwa kawaida viambishi vinapopachikwa kwenye mzizi au shina la neno huwakilisha dhima mbalimbali kama vile nafsi, hali, njeo, idadi, yambwa, urejeshi, ngeli, ukanushi, dhamira mbalimbali, masharti, kauli mbalimbali za vitenzi, pamoja na kuunda kategoria mpya za maneno ili kuongeza msamiati wa lugha (Nkwera, 1989). Kwa mfano, katika (1a) kiambishi awali **a-** kinawakilisha nafsi, kiambishi **-na-** kinawakilisha njeo, **-wa-** kinawakilisha yambwa, **-esh-** kinawakilisha hali utendeshi na **-a** kinawakilisha dhamira elezi yakinishi. Katika (1b) kiambishi **si-**

kinawakilisha ukanushi na kiambishi **-i** kinawakilishaa dhamira kanushi. Katika (1c) kiambishi **-sh-** kinawakilisha utendeshi na kimebadili kategoria ya kivumishi *refu* kuwa kitenzi *refusha*. Kiambishi **-o** katika mfano (1d) ni kinominishi kimebadili kitenzi *soma* kuwa nomino *somo.* Katika mfano (1e) kiambishi **m-** kinawakilisha ngeli. Wakati mwingine kiambishi kimoja kinaweza kuwa na dhima zaidi ya moja. Kwa mfano kiambishi **-wa-** katika (1a) kinawakilisha yambwa, idadi na nafsi.

Mchakato wa kupachika viambishi kabla na baada ya mzizi huitwa uambishaji. Kwa maneno mengine tunaweza kusema kwamba uambishaji ni utaratibu wa kuweka viambishi kabla, katikati au baada ya mzizi wa neno (Massamba, 2004:89). Hata hivyo, Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu haziruhusu upachikaji wa viambishi katikati ya mzizi au shina la neno kwa sababu mizizi au mashina yake hayawezi kugawika bila kupoteza maana. Uambishaji umegawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni unyambulishaji na uambatizi (Peterson, 2008; Kahigi, 2009). Unyambulishaji ni uambishaji wenye dhima ya kubadili maana au kategoria ya neno ilhali uambatizi ni uambishaji wenye dhima za kisarufi (Spencer na Zwicky, 1998; Kahigi, 2009). Mgawanyo huo ulifanywa katika lugha za Ulaya kwa kuwa sarufi yake ilikuwa imefafanuliwa na kuandikwa (Kosch, 2011). Kosch anaendelea kueleza kuwa, data kutoka lugha mahususi hasa zisizo za asili ya Ulaya zinapingana na mgawanyo huo. Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu ni miongoni mwa lugha ambazo data yake inapingana na mgawanyo huo kwa sababu haiwezi kutofautisha unyambulishaji na uambatizi. Mfumo wa ngeli za nomino wa lugha za Kibantu ni mfano mzuri wa muingiliano kati ya unyambulishaji na uambatizi (Kosch, 2011). Hata katika mofolojia ya kategoria nyingine za maneno kama vitenzi na vivumishi unyambulishaji na uambatizi huingiliana. Mwingiliano huo ni miongoni mwa mambo ambayo huibua utata katika lugha ya Kiswahili. Katika makala hii tumeonesha utata huo kwa mifano na kusisitiza kuwa ufafanuzi wa sarufi ya lugha ya Kiswahili hauwezi kukamilika bila kutambua utata huo.

### Utata katika Matumizi ya Dhana za Unyambulishaji na Uambatizi

Katika sehemu hii tumejadili masuala matatu ambayo yanaibua utata katika matumizi ya dhana za unyambulishaji na uambatizi katika ufafanuzi wa sarufi ya Kiswahili. Masuala hayo ni dhima za viambishi vya unyambulishaji na uambatizi, nafasi ya viambishi vya unyambulishaji na uambatizi katika mzizi au shina la neno, na tatu istilahi zinazotumika kurejelea dhana au michakato ya unyambulishaji na uambatizi.

### Dhima za Unyambulishaji na Uambatizi

Dhima ni kigezo kimojawapo kinachotumika kutofautisha mchakato wa unyambulishaji na uambatizi. Mchakato wa unyambulishaji una dhima ya kubadili maana au kategoria ya neno wakati uambatizi haubadili maana wala kategoria ya neno bali una dhima ya kuongeza nduni za kisarufi tu katika neno husika (Katamba, 1993; Spencer na Zwicky, 1991). Dhima hizi hubebwa na viambishi vya michakato hiyo. Viambishi vya unyambulishaji vinapopachikwa kwenye mzizi au shina la neno vinaweza kubadili kategoria au maana ya neno wakati viambishi vya uambatizi vina dhima za kisarufi kama kuonesha idadi, njeo, hali, dhamira, nafsi, ngeli, yambwa, urejeshi, ukanushi na kadhalika. Kwa ufafanuzi zaidi tazama mifano Na. 2 na 3.

**Mfano 2: Viambishi nyambulishi**

| | Vitenzi | Nomino nyambuo | Utendana | Utendesha | Utendwa | Utendea |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (a) | soma | pig-**o** | pig-**an**-a | pig-**ish**-a | pig-**w**-a | pig-**i**-a |
| (b) | cheka | chek-**o** | chek-**an**-a | chek-**esh**-a | chek-**w**-a | chek-**e**-a |

**Mfano 3: Viambishi ambatizi**

| | Shina | Viambishi ambatizi |
|---|---|---|
| (a) | soma | **wa-na-o**-som-**a** |
| (b) | piga | **ha-tu-m**-pig-**i** |
| (c) | refu | **m**-refu |

Katika mifano (2a) na (b) kiambishi **-o** ni kiambishi cha unyambulishaji kwa sababu, kimebadili kategoria ya neno. Awali, maneno hayo yalikuwa ni vitenzi lakini baada ya kuwekewa kiambishi **-o** yamebadili kategoria na kuwa nomino. Pia, viambishi vingine vilivyokolezwa wino katika mifano hiyo ni vya unyambulishaji kwa sababu vimebadili maana ya neno. Kwa mfano, awali kitenzi cheka maana yake ni 'toa sauti ya furaha au ya dharau kwa kufunua kinywa hadi meno yaonekane' (TUKI, 2004). Kwa kuongezewa viambishi **-an-**, cha kutendana, **-esh-** cha utendesha, **-w-** cha utendwa, na kiambishi **-e-** cha utendea maana ya awali ya kitenzi cheka imepanuka zaidi. Kwa mujibu wa kamusi ya TUKI (2004) kitenzi "chekesha" maana yake ni 'fanya mtu au watu wacheke.' Aidha, viambishi vilivyokolezwa wino katika mifano (3a-c) ni viambishi vya uambatizi kwa sababu vina dhima za kisarufi. Kwa mfano, katika (3a), kiambishi **wa-** kinawakilisha nafsi ya tatu wingi, **-na-** kinawakilisha njeo wakati uliopo, **-o-** kinawakilisha urejeshi, na **-a** kinawakilisha dhamira elezi yakinishi.

Ingawa mifano hiyo inaonyesha kuwa dhana ya unyambulishaji na uambatizi iko bayana, lakini ieleweke kwamba sio kila wakati kigezo hiki cha dhima kinaweza kutofautisha michakato hiyo bila kuleta utata. Kuna wakati kiambishi kimoja kinafanya kazi ya kisarufi na wakati huo huo kinabadili maana au kategoria ya neno. Tazama mifano ifuatayo Na. 4.

**Mfano 4: Viambishi ambatizi na nyambulishi**

| | **Mfano** | **Maana** | **Ngeli** |
|---|---|---|---|
| (a) | **m**-toto | mtu mwenye umri mdogo | ngeli ya 1 |
| | **u**-toto | hali au tabia kama ya mtoto | ngeli ya 14 |
| | **ki**-toto | udogeshi wa nomino mtoto | ngeli ya 7 |
| (b) | **M**-swahili | mtu | ngeli ya 1 |
| | **Ki-**swahili | lugha | ngeli ya 7 |
| | **u**-swahili | hali | ngeli ya 14 |
| (c) | **m-**tu | binadamu | ngeli ya 1 |
| | **u**-tu | hali ya ubinadamu | ngeli ya 14 |
| | **ki**-tu | chochote kisicho hisivu | ngeli ya 7 |
| | **ji**-tu | ukubwa wa nomino mtu | ngeli ya 5 |

Chanzo: TUKI (2004)

Viambishi vilivyokolezwa wino katika mifano (4a-c) ni viambishi ngeli ambavyo ni vya uambatizi, viambishi hivyohivyo vimenyambulisha nomino hizo kwa kubadili maana na ngeli za nomino hizo. Kuthibitisha kuwa nomino hizo zimebadili maana, zimeingizwa kwenye kamusi kama vidahizo tofauti. Huo ni mfano wa unyambulishaji wa nomino kwa kubadili ngeli. Kahigi (2009) anaeleza kwamba unyambulishaji wa namna hii hutokea pindi shina la nomino linapotumika na kiambishi ngeli zaidi ya kimoja. Kwa maana hiyo, viambishi vilivyokolezwa wino ni vya uambatizi kwa kuwa vina dhima za kisarufi yaani kuwakilisha ngeli na ni vya unyambulishaji kwa kuwa vimenyambulisha nomino zikabadili maana na ngeli. Huu ni mfano wa muingiliano kati ya unyambulishaji na uambatizi. Kutokana na muingiliano huo tunaweza kusema mfumo wa ngeli wa lugha ya Kiswahili si wa uambatizi peke yake, bali ni wa uambatizi na unyambulishaji. Kutokana na hali hiyo, kigezo cha dhima za viambishi vya unyambulishaji na uambatizi kinaibua utata katika ufafanuzi wa sarufi ya Kiswahili kwa sababu kiambishi kimoja kinaweza kuwa cha uambatizi na unyambulishaji.

Vilevile, viambishi vya uambatizi vinaweza pia kubadili kategoria ya neno. Hali hii inazidi kuibua utata kwa kuwa inakuwa vigumu kutofautisha unyambulishaji na uambatizi. Chunguza mifano ifuatayo namba (5a-c).

**Mfano 5: Viambishi ambatizi na nyambulishi**

| | Mifano ya mashina ya maneno | Nomino nyambuo | Ngeli |
|---|---|---|---|
| (a) | pika | **ku**-pika | ngeli 15 |
| | lala | **ku**-lala | ngeli 15 |
| | imba | **ku**-imba | ngeli 15 |
| (b) | ratibu | **m**-ratibu | ngeli ya 1 |
| | hubiri | **m**-hubiri | ngeli ya 1 |
| | saliti | **m**-saliti | ngeli ya 1 |
| | talii | **m**-talii | ngeli ya 1 |
| (c) | zuri | **u**-zuri | ngeli ya 14 |
| | baya | **u**-baya | ngeli ya 14 |
| | refu | **u**-refu | ngeli ya 14 |
| | nene | **u**-nene | ngeli ya 14 |

Chanzo: TUKI (2014)

Katika (5a) kiambishi ngeli **ku-** kimebadili kategoria ya vitenzi na kuwa nomino zinazoingia katika ngeli ya 15. Hii ina maana kiambishi **ku-** ni kiambishi ambatizi kwa kuwa kinawakilisha ngeli na ni kiambishi nyambulishi kwa kuwa kinabadili vitenzi kuwa nomino. Tukichunguza mfano wa (5b) tunabaini kuwa kiambishi **m-** cha ngeli ya kwanza ambacho ni cha uambatizi kimeweza kubadili vitenzi kuwa nomino. Hata hivyo, tunaweza kusema hali hiyo imetokea kwa sababu vitenzi hivyo sio vya Kibantu kwa sababu haviishii na irabu **-a** kama ilivyo ada kwa vitenzi vya Kibantu. Lakini kwa kuwa vitenzi hivyo tayari vimeingizwa katika lugha ya Kiswahili hatuwezi kuvitenga katika ufafanuzi wa sarufi ya Kiswahili. Hivyo, tunapounda maneno mapya kutokana na vitenzi hivyo kwa kutumia mchakato wa unyambulishaji na uambatizi tunapata utata kwa kuwa kiambishi ngeli ambacho ni cha uambatizi kinaweza kubadili kategoria ya vitenzi hivyo kuwa nomino. Hali hii inaleta utata kwa sababu tunashindwa kutofautisha viambishi vya unyambulishaji na vile vya uambatizi katika sarufi ya Kiswahili. Fauka ya hayo, katika mfano wa (5c) tunabaini kuwa kiambishi **u-** cha ngeli ya 11 kimebadili kategoria za vivumishi kuwa nomino. Mifano hiyo inaonesha kuwa vivumishi vinaweza kunyambulishwa na kuzalisha nomino (Kahigi, 2009). Katika hali kama hiyo, ni vigumu kuweka mpaka kati ya unyambulishaji na uambatizi katika ufafanuzi wa sarufi ya Kiswahili kwa sababu kiambishi kimoja kinabeba dhima za uambatizi na unyambulishaji.

Aidha, viambishi vingine vya uambatizi kama kiambishi **ji-** cha kujirejea, hubadili maana ya baadhi ya vitenzi. Kiambishi hiki kimekuwa sehemu ya mizizi ya vitenzi hivyo kwani haviwezi kutengwa tena na mizizi hiyo bila vitenzi hivyo kupoteza maana. Tazama mfano namba (6) kwa ufafanuzi zaidi:

**Mfano 6: Kiambishi ambatizi ji- kinavyonyambulisha vitenzi kwa kubadili maana**

| | Kitenzi cha awali | Maana ya awali | Kitenzi kipya | Maana mpya |
|---|---|---|---|---|
| (a) | tapa | linatokana na neno tapatapa lenye maana babaika | **ji**tapa | jisifu kwa kujiona bora zaidi |
| (b) | ona | tambua kitu kwa macho | **ji**ona | kuwa na majivuno; ringa, takabari |
| (c) | vuna | toa mazao shambani | **ji**vuna | hisi kuwa una zaidi kuliko wengine jiona bora, ringa |
| (d) | fungua | acha wazi | **ji**fungua | hali ya kuzaa (kwa binadamu) |
| (e) | gamba | ngozi kama pembe au ngozi ngumu ya kasa au samaki | **ji**gamba | Jifanya unajua sana; jifutua; jifaragua; jikita; jinadi; jibodoa; jivuna; jinaki |

Chanzo: TUKI (2004)

Tukichunguza mifano hiyo, maana ya awali ya vitenzi hivyo kabla ya kuwekewa kiambishi **ji-** ni tofauti kabisa na maana ya vitenzi hivyo baada ya kuwekewa kiambishi **ji-** cha kujirejea. Kiambishi hiki kwa kawaida ni cha uambatizi lakini katika mifano hiyo tunaona kimebadili kabisa maana ya kitenzi cha awali. Tena kiambishi hicho kimeganda katika mizizi ya vitenzi hivyo na kimekuwa sehemu ya vitenzi hivyo na ndio maana vitenzi hivyo huingizwa kwenye kamusi kama vidahizo tofauti. Hata hivyo, sio vitenzi vyote hubadili maana kwa kuwekewa kiambishi **ji-** cha kujirejea kama ambavyo mfano wa (7) unaonesha hapa chini:

**Mfano 7: Kiambishi ambatizi ji- hakibadili maana ya vitenzi**

| | **Shina na kitenzi kabla ya kuwekewa kiambishi ji-** | **Maana** | **Shina la kitenzi baada ya kuwekewa kiambishi -ji** |
|---|---|---|---|
| (a) | ua | ondoa uhai wa kitu au mtu | **ji**ua |
| (b) | kata | pitisha kitu chenye makali kwenye kitu | **ji**kata |
| (c) | choma | ingiza kitu chenye ncha ndani ya ngozi au nyama au kitu chochote laini | **ji**choma |
| (d) | pamba | tia mapambo katika kitu ili kipendeze machono | **ji**remba |

Chanzo: TUKI (2004)


Tukichunguza vitenzi vilivyotolewa katika mfano Na. (7) tutabaini kuwa kiambishi **ji-** kimefanya kazi ya kisarufi kuonesha hali ya kujirejea tu, lakini hakikubadili maana za vitenzi. Hata baada ya kuwekewa kiambishi **ji-** vitenzi hivyo havikuingizwa tena kwenye kamusi kama vidahizo kwa kuwa havikubadili maana. Hali hii ni tofauti na ile tuliyoiona awali katika mfano Na. 6 ambapo vitenzi vilipowekewa kiambishi **ji-** vilibadili maana na kuingizwa kwenye kamusi kama vidahizo vipya.

Hivyo, kutokana na maelezo na mifano tuliyoiona, ni dhahiri kuwa kigezo cha dhima za unyambulishaji na uambatizi hakiwezi kutofautisha michakato hiyo katika lugha ya Kiswahili. Hali hii huibua utata kwa sababu kiambishi kimoja kinaweza kubeba dhima ya uambatizi na unyambulishaji. Hali hii imekuwa ikiwasumbua wanafunzi katika kozi za mofolojia kwa sababu kiambishi kimoja kinaweza kuwa na dhima za kisarufi na dhima ya kubadili maana au kategoria ya neno kwa pamoja. Hivyo, makala hii inapendekeza kuwa tunapofasili au kutumia dhana ya uambatizi na unyambulishaji katika sarufi ya Kiswahili ni muhimu kueleleza kuwa wakati mwingine ni vigumu kuweka mpaka baina ya dhana hizi. Yaani, kiambishi kimoja kinaweza kuwa na dhima ya kisarufi (uambatizi) na dhima ya kubadili maana au kategoria ya neno (unyambulishaji).

**Nafasi ya Viambishi katika Mzizi au Shina la Neno**

Baadhi ya wataalamu wa Kiswahili kama vile Mgulu (1999), Nkwera (1989), Kihore na wenzake (2003) na Gawasike (2012) kwa kutaja wachache, hutumia kigezo cha mzizi kuweka mpaka au kutofautisha unyambulishaji na uambatizi. Suala hili linazidi kuibua utata. Kwa mfano, Nkwera (1989) anaeleza kuwa viambishi maana, yaani viambishi ambatizi, hutokea mwanzoni, kati au mwisho wa mzizi, na viambishi vijenzi akimaanisha viambishi vya unyambulishaji hutokea hasa mwishoni mwa mzizi. Naye Mgullu (1999) anadai kuwa viambishi vya mnyumbuliko wa maneno akimaanisha uambatizi hupachikwa kabla ya mzizi, na vile vya uundaji wa maneno akimaanisha unyambulishaji hupachikwa baada ya mzizi. Gawasike (2012) anaeleza kuwa, mzizi ndio mpaka wa mgawanyo wa uambatizi na unyambulishaji. Anaendelea kueleza kuwa, katika lugha ya Kiswahili na lugha za Kibantu kwa ujumla unyambulishaji ni uongezaji wa mofu au viambishi baada ya mzizi wa neno na uambishaji akimaanisha (uambatizi) ni uongezaji wa mofu/viambishi kabla ya mzizi. Maelezo hayo anayaweka katika kielelezo kifuatacho:

**Kielelezo 1: Mpaka kati ya uambatizi na unyambulishaji**




Gawasike (2012:73)

Kwa kutumia kielelezo hicho Gawasike anaonyesha wazi kuwa mzizi ndiyo mpaka wa uambatizi na unyambulishaji. Hivyo, viambishi vyote vya uambatizi hutokea kabla ya mzizi na vile vya unyambulishaji baada ya mzizi. Mawazo ya Gawasike (2012) yanafanana na yale ya Kihore na wenzake (2003) ambao wanaeleza kwamba uambatizi unaweza kutokea kabla ya mzizi wa neno pekee na unyambulishaji hutokea baada ya mzizi.

Tukichunguza fasili hizo tunaona kuwa zote zinataja mzizi kama kigezo cha kutofautisha uambatizi na unyambulishaji. Matumizi ya kigezo cha kabla na baada ya mzizi kutofautisha michakato hiyo yanazidi kuibua utata kwa sababu katika lugha ya Kiswahili na baadhi ya lugha nyingine za Kibantu ni vigumu kutenganisha viambishi vya unyambulishaji na vile vya uambatizi kwa kutumia kigezo cha mzizi kama mpaka. Tazama mfano ufuatao Na. 8.

**Mfano 8: Viambishi ambatizi baada ya mzizi**

| | **Mfano** | **Viambishi vya dhamira kwenye vitenzi** |
|---|---|---|
| (a) | lima | silim-**i** |
| (b) | pika | upik-**e** |
| (c) | soma | ninasom-**a** |
| (d) | imba | imb-**eni** |
| (e) | simama | simam-**eni** |

Chanzo: Nkwera (1989:69)

Katika mfano wa (8) viambishi vilivyokolezwa wino vinaonyesha dhamira ya mzungumzaji. Dhamira ni kipengele mojawapo cha kisarufi ambacho huhusu uchanganuzi wa nia mbalimbali katika kitenzi ambazo hubainisha lengo la msemaji kama vile kutoa taarifa, kuamuru, kusihi au kukataa (Nkwera, 1989; Peaterson, 2008). Hii ina maana viambishi hivyo ni vya uambatizi na huwekwa baada ya mzizi. Katika mfano (8a) kiambishi **-i** kinawakilisha dhamira kanushi, kiambishi **-e** katika (8b) kinawakilisha dhamira amrishi na kiambishi **-a** katika (8c) kinawakilisha dhamira elezi yakinishi. Viambishi **-eni** katika (8d) na (8e) vinawakilisha dhamira amrishi nafsi ya pili wingi. Viambishi hivyo ni vya uambatizi ingawa hutokea baada ya mzizi tofauti na fasili za wataalamu tuliowataja ambao wanaeleza kuwa viambishi ya uambatizi hutokea kabla ya mzizi.

Hata hivyo, tunaweza kupata mifano zaidi katika lugha nyingine za Kibantu ambazo viambishi vya uambatizi kama vya njeo na hali hutokea baada ya mzizi. Hali hii inajidhihirisha katika lugha mbalimbali za Kibantu kama vile Kimashami, Kisukuma, Kinyamwezi, Kigogo na Kikuria. Hali hii inaonesha wazi kuwa si kweli kwamba katika lugha ya Kiswahili na lugha zote za Kibantu viambishi vya uambatizi hutokea au hupachikwa kabla ya mzizi kama alivyoeleza Gawasike (2012). Mfano (9) umetoka katika lugha ya Kigogo ambapo katika lugha hiyo viambishi vya njeo na hali huweza pia kutokea baada ya mzizi wa kitenzi.

**Mfano 9: Viambishi ambatizi vya njeo na hali kabla na baada ya mzizi**

| | Kigogo | Kiswahili |
|---|---|---|
| (a) | ***si-ya****-tol-****il-e*** | hakuoa |
| (b) | ***ya****-gon-****il-e*** | amelala |
| (c) | ***i****-dod-****il-e*** | imeoza |
| (d) | ***si-ci-a****-lim-****ag-a*** | tulizoea kulila |
| (e) | ***si-ci-a****-telek-****ag-a*** | tulizoea kupika |

Chanzo: Rugemalira (2014:66)


Katika mifano hiyo viambishi vilivyokolezwa wino ni viambishi vya uambatizi vyenye dhima ya kuonesha hali na njeo na hutokea kabla ya mzizi na baada ya mzizi. Kiambishi **-il-** katika (9a-c) ni kiambishi cha hali timilifu ilhali kiambishi **-ag-** katika (9d) na (e) ni kiambishi cha hali ya mazoea. Irabu ishilizi, yaani **-e** na **-a,** ni viambishi vya dhamira. Kwa mifano hiyo, ni dhahiri kuwa kigezo cha kabla na baada ya mzizi hakiwezi kutofautisha dhana ya unyambulishaji na uambatizi katika sarufi ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu badala yake huibua utata. Hii ni kwa sababu viambishi ambatizi na viambishi nyambulishi huweza kutokea kabla na baada ya mzizi au shina.

Kutokana na hali hiyo, makala hii inapendekeza fasili ya uambatizi iwe ni upachikaji wa viambishi katika mzizi au shina la neno vyenye dhima ya kisarufi ilhali unyambulishaji ni upachikaji wa viambishi katika mzizi au shina la neno vyenye dhima ya kubadili maana au kategoria ya neno. Aidha, ni muhimu kusisitiza kuwa kiambishi kimoja kinaweza kuwa cha uambatizi na unyambulishaji. Mzizi au shina visitumike kama mpaka kwa sababu viambishi vya uambatizi na unyambulishaji vinaweza kutokea kabla na baada ya mzizi.

### Istilahi Zinazotumiwa Kurejelea Unyambulishaji na Uambatizi katika Lugha ya Kiswahili

Miongoni mwa mambo yanayoibua mkanganyiko au utata ni pamoja na istilahi zinazotumiwa na wataalamu wa Kiswahili kurejelea dhana ya uambishaji, unyambulishaji na uambatizi. Miongoni mwa wanaisimu hao ni pamoja na Nkwera (1989), Rubanza (1996), Mgullu (1999), Massamba (2004) na Gawasike (2012) kwa kutaja wachache. Gawasike (2012) anaeleza kwamba dhana za uambishaji, uambatizi na unyambulishaji katika lugha ya Kiswahili zimezungumziwa kwa namna tofauti tofauti na wanaisimu waliotangulia. Miongoni mwa tofauti hizo ni pamoja na istilahi zinazotumiwa na wanaisimu hao kurejelea dhana hizo. Mathalani, Nkwera (1989) anatumia dhana ya **viambishi maana** akirejelea uambatizi na **viambishi vijenzi** akirejelea unyambulishaji. Nkwera anaeleza kwamba viambishi maana hutokea mwanzoni au mwishoni mwa shina la neno. Viambishi hivi hutanua maana bila ya kubadilisha shina au mzizi wa neno. Viambishi vijenzi hutokea hasa mwishoni mwa mzizi wa neno na hutanua maana au kubadili kategoria ya neno. Anaendelea kueleza kuwa uwezo wa mzizi au shina kufungiwa viambishi hivyo mwanzoni au mwishoni huitwa mnyambuliko. Kwa upande wake, Rubanza (1996) anatumia istilahi ya **unyambulishaji** akirejelea uambishaji na anafasili kuwa ni upachikaji wa mofimu katika mzizi wa neno. Anaendelea kueleza kuwa **unyambulishaji** (uambishaji) unaweza kuwekwa katika makundi mawili ambayo ni **uambishaji** akimaanisha (uambatizi) na **unyambuaji** akimaanisha unyambulishaji. Naye Mgullu (1999) anatumia dhana ya **minyumbuliko ya maneno** akimaanisha uambatizi na **uundaji wa maneno** akimaanisha unyambulishaji. Anaendelea kueleza kuwa, viambishi vya mnyumbuliko wa maneno (uambatizi) hupachikwa kabla ya mzizi na vile vya uundaji wa maneno (unyambulishaji) hupachikwa baada ya mzizi. Massamba (2004) anafasili uambishaji kuwa ni taaluma ya mofolojia inayohusu utaratibu wa kuweka kiambishi kabla, katikati au baada ya mzizi. Anabainisha kuwa kuna aina mbili za uambishaji ambazo ni **uambishaji nyambulishi** akimaanisha unyambulishaji, na **uambishaji kisarufi** akimaanisha uambatizi. Wataalamu wengine ni Nyangwine na Masebo (2007) ambao wanatumia dhana ya **uambishaji** wakimaanisha uambatizi kuwa ni upachikaji wa mofimu katika mzizi ili kuleta upatanisho wa kisarufi. Istilahi wanazotumia wataalamu hao tumeziweka kwenye vielelezo vifuatavyo kwa ufafanuzi zaidi.


**Kielelezo 2: Istilahi zinazotumiwa na wataalam mbalimbali**




Vielelezo hivyo, vinaonesha baadhi ya wataalamu walioeleza kuhusu unyambulishaji na uambatizi katika lugha ya Kiswahili. Tukichunguza vielelezo hivyo tunaona namna wataalamu hao wanavyotofautiana kutokana na istilahi wanazozitumia kurejelea michakato hiyo. Kutokuwa na istilahi bainifu za kurejelea michakato hiyo kunaibua hali ya mkanganyiko au utata. Hali hii pia inaonesha kuwa ni vigumu kutofautisha michakato hiyo katika lugha ya Kiswahili. Hivyo, kama anavyoeleza Gawasike (2012) kuna umuhimu wa kuwa na istilahi rasmi au bainifu za kurejelea michakato hiyo ili zitumike miongoni mwa wanaisimu wote wa Kiswahili kama ilivyo katika Kiingereza. Wataalamu wengine waliozungumzia dhana hizi katika lugha ya Kiswahili ni pamoja na TUKI (1990) na Kihore na wenzake (2003).

Hata hivyo, Gawasike (2012) alipendekeza itumike istilahi ya **uambikaji** kurejelea mchakato wa kupachika viambishi katika mzizi au shina la neno. **Uambikaji** huo umegawanyika katika matawi mawili ambayo ni **unyambulishaji** na **uambishaji** (uambatizi). Tazama kielelezo Na. 3 kwa ufafanuzi zaidi.

**Kielelezo 3: Istilahi zilizopendekezwa na Gawasike**




Tukichunguza istilahi zilizopendekezwa na Gawasike (2012) bado zinaibua utata kwa sababu hakuna tofauti kati ya *uambikaji* na *uambishaji* zaidi ya tofauti ya kauli tu kwamba uambikaji ni utendeka na uambishaji ni usababishi. Ndio maana katika kamusi maneno yenye mahusiano hayo hayaingizwi kama vidahizo viwili tofauti badala yake huingizwa ndani ya kidahizo kimoja. Kwa mfano, katika kamusi ya TUKI (2004) kuna kidahizo *uambishaji* na kauli nyingine zinatajwa ndani ya kidahizo hicho. Kutokana na hali hiyo, istilahi hizo hazitoshi kutofautisha michakato miwili bila kuibua mkanganyiko kwa sababu wakati mwingine istilahi ya *uambikaji* na *uambishaji* hutumika kama vibadala. Hata hivyo, Gawasike (2012) hakueleza kwa nini anapendekeza istilahi ya *uambishaji* itumike kurejelea uambatizi na hakuonyesha upungufu au matatizo ya kutumia istilahi ya uambatizi.

Katika makala hii tunapendekeza istilahi ya jumla iwe ni *uambishaji* ambayo kwa mujibu wa TUKI (2004) ni upachikaji wa viambishi katika mzizi wa neno. Istilahi hii imekuwa ikitumiwa hivyo na wataalamu kama (Nkwera, 1989; Massamba, 2004 na Kahigi, 2009). Vilevile, katika makala hii tunaunga mkono matumizi ya istilahi ya unyambulisha*ji* kurejelea upachikaji wa viambishi katika mzizi au shina la neno vyenye dhima ya kubadili maana au kategoria ya neno na *uambatizi* kuwa ni upachikaji wa viambishi kwenye mzizi au shina vyenye dhima ya kuongeza nduni za kisarufi. Istilahi hizo zimekuwa zikitumiwa hivyo na baadhi ya wataalamu kama Peterson (2008) na Kahigi (2009). Tunapendekeza istilahi ya *uambatizi* iendelee kutumika kwa sababu maana yake inasawiri dhana hiyo ya upachikaji wa viambishi vya kisarufi katika mzizi au shina la neno. Neno *uambatizi* limetokana na neno *ambata* ambalo lina maana ya kushikanisha kitu na kingine na *ambatisha* lina maana ya ongeza au bandika kitu cha ziada kwenye kitu kingine (TUKI, 2004). Tunapobandika viambishi vyenye dhima za kisarufi katika mzizi au shina la neno, viambishi hivyo huongeza taarifa ya ziada kwa sababu mara nyingi havibadili maana ya neno au kategoria ya neno husika. Aidha, neno *unyambulishaji* kwa mujibu wa TUKI (2004) ni kitendo cha kuongeza kiambishi kwenye mzizi wa neno ili kupata neno jingine la kategoria ile ile au kategoria nyingine tofauti. Kielelezo Na. 4 kinawakilisha mapendekezo ya makala hii juu ya istilahi

za kutumia kurejelea michakato hiyo.

**Kielelezo 4: Istilahi zilizopendekezwa katika sura hii**




Pamoja na mapendekezo hayo, ieleweke kuwa dhana ya uambatizi na unyambulishaji zinatumika kurahisisha ufafanuzi wa sarufi ya Kiswahili ingawa wakati mwingine ni vigumu kutofautisha michakato hiyo hasa pale kiambishi kimoja kinapofanya kazi ya kisarufi na kubadili maana au kategoria ya neno.

**Hitimisho**

Makala hii imebaini kwamba kuna utata katika kutumia dhana za unyambulishaji na uambatizi katika ufafanuzi wa sarufi ya Kiswahili. Hii inatokana na ukweli kwamba mpaka dhahiri kati ya unyambulishaji na uambatizi hauwezi kuonekana wakati wote. Aidha, dhana hizi ni muhimu katika kurahisisha ufafanuzi wa sarufi ya Kiswahili kwa sababu viambishi vinavyopachikwa kwenye maneno havina dhima au hadhi moja bali vina dhima tofauti kama vile kubadili maana ya neno au kubadili kategoria ya neno pamoja na dhima za kisarufi. Hivyo, ili kurahisisha ufafanuzi wa sarufi ya Kiswahili ni muhimu kuweka bayana ni viambishi vipi vinavyoweza kubadili maana na kategoria ya neno na vile vinavyofanya kazi za kisarufi. Hata hivyo, ni muhimu kuweka bayana kuwa wakati mwingine kiambishi kimoja kinaweza kubeba dhima zote hizo hali inayoleta ugumu katika kuweka mpaka dhahiri kati ya dhana hizo. Aidha, kigezo cha kabla na baada ya mzizi kisitumike kutofautisha

uambatizi na unyambulishaji kwa sababu kigezo hicho kinazidi kuibua utata kama tulivyoona. Vilevile, ni muhimu wanaisimu wa lugha ya Kiswahili kutumia istilahi bainifu kurejelea dhana hizo ili kupunguza mkanganyiko.

**Marejeo**

Ashton, E.O. (1947). *Swahili Grammar* (Including Intonation). London: Longman.

Booij, G. (2006). Inflection and Derivation. In Keith Brown, *Encyclopedia of Language & Linguistics*, Second Edition, volume 5, pp. 654-661.

Gawasike, A. (2012). "Dhana ya Uambikaji Katika Kiswahili". *Kioo cha Lugha*. Juz.10:70-78. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TATAKI.

Kahigi, K. (2009). "Unyambulishi wa Nomino na Vitenzi katika Kikahe". *Kioo cha Lugha*. Juz.7:1-10. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TATAKI.

Katamba, F. (1993). *Morphology*. London: The Macmillan Press Ltd.

Kihore, Y.M. (2011). Majibu kwa Makala "Mkanganyiko wa Dhana za Mzizi, Kiini na Shina" Yaliyoandikwa na Joash J. Gambarage. *Kiswahili*. Juz. 74. 25-27. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TATAKI.

Kihore, Y. M na Wenzake. (2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI

Kosch, I. (2011). Descriptive issues of derivation and inflection in Sesotho, In *Southern African Linguistics and Applied Language Studies,* 29:1, 89-96.

Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI

Mgullu, R. (1999). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Kampala: Longhorn Publishers Ltd.

Nkwera, V. F. (1989). *Sarufi na Fasihi: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: Creative Prints Ltd.

Nyangwine, N. na J.A. Masebo. (2007). *Nadharia ya Lugha ya Kiswahili: Kidato cha 5&6*. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.

Peterson, R. (2008). "Baadhi ya Vipengele vya Uambatizi wa Vitenzi katika Kishambala". *Kioo cha Lugha*. Juz. 6. 52-62. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TATAKI.

Rugemalira, J. (2004). Sarufi ya Kigogo: Rasimu ya Awali (Haijachapwa).

Spencer, A. & Zwicky, A. (1998). *The Handbook of Morphology*. Stanford University and Ohio State University: Blackwell Publishers Ltd.

Rubanza, Y. I. (1996). *Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

TUKI. (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press.